

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION  
(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,  
AMAGORO CONSTITUENCY,  
AT ALUPE HALL.**

**ON**

**2<sup>nd</sup> August 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,**  
**AMAGORO CONSTITUENCY,**  
**HELD AT ALUPE HALL ON AUGUST 2<sup>ND</sup> 2002.**

**Present.**

Com. Pastor Zablon Ayonga

Com. Dr. Abdirizak Nunow

Com. Mutakha Kangu- chair

**Secretariat Staff Attendance:-**

Samuel Wanjohi - Programme Officer  
Hellen Namisi - Asst. Programme Officer  
Grace Gitu - Verbatim Recorder  
Charles Angedu Akisa - Distirict Co-ordinator

Meeting started at 9:40 am with Com. Mutakha Kangu.

**Charles Ekisa:** Chairman of the Constitutional Committee Teso, support team, the leaders of Teso County Council, ladies and Gentlemen, good morning. We would like to begin our session with a word of prayer. Mr. Adungo if you could lead us.

**Mr. Adungo: (prayers)**Let us bow down for prayers; in the name of the Father and the Son and the Holy Spirit Amen, Lord now we are here together for a very great purpose of this Nation. Lord, become our chairman and guide us, guide the Commissioners and guide the participants and the contributors so that whatever we are going to present should be very good for this Nation. Lord unless you are there in front of us we cannot do anything good, Lord it is all for you today and you become our Chairman, I ask all this through Christ our Lord, Amen.

**Charles Ekisa:** Asanti sana Bwana Adungo kwa majina mimi naitwa Charles Angedu the

District Co-ordinator for the CKRC in Teso. Ningependa kuchukuwa nafasi hii kukaribisha Commissioners wetu katika Wilaya ya Teso wamekua nasi tangu jana na leo hii tuna bahati kuwa katika taarafa moja ya Wilaya ya Teso, inayoitwa Chakol Division. Mjisikie muko nyumbani kabisa na kazi ilio mbele yetu kila mmoja anaelewa ya kwamba serikali yetu tukufu iliamua ya kwamba Wanakenya washirikishwe katika jambo hili la kurekebisha Katiba hii yetu. Watu wa Chakol muko na nafasi nzuri leo hapa kutoa maoni yenu kuhusiyana na mambo haya. Na kwa ukweli ni siku ya kutowa maoni sio mambo mengine, kwa sababu tumekuwa elimu ya uraia kuhusiana na jambo hili na tumefanya katika kila location, katika taarafa hii na tuna amini ya kwamba nyinyi muko tayari kabisa kuwasilisha maoni yenu kwa Commission.

Vile mlikuwa mkiingia kuna form imekuwa kule nje ya registration, tafadhali uhakikishe kwamba jina lako limewakilishwa katika hiyo form. Hiyo form ndio itatumiwa kukuita wewe hapa uweze kupeana maoni yako. Na ningeomba watu wa Chakol, watu wa Amagoro jana walifanya vizuri sana kwa sababu walikuwa wakiongea mambo yao kinaganaga na ningependa nanyi pia mfuata huo mtindo. Commissioners wetu watatupatia utaratibu tutakao fuata katika kikao cha leo. Tukifirikira ya kwamba tuko na Mungu mbele yetu atatuongoza katika mambo hayo yote na ninawaombea kikao kizuri katika wilaya ya Teso. Tuko hapa na Chairman wa Constituency Constituional Committee, ningependa kumuona yeye aseme jambo moja ili akaribishe Chairman wa County Council pia kwa sababu tuko kwake, aweze kukaribisha wageni. Karibu Chairman.

**3C's Chairman Samson Olubayi:** Commissioners wetu, Bwana DO wa Chakol division, Co-ordinator, Chairman County Council, viongozi kwa jumla ambao tuko hapa pamoja kutoka tabaka mbali mbali pamoja na sisi kwa jumla. (Teso dialect).

Kwa hivyo nimekata tu short salamu ya kinyumbani, kw hivyo kutoka hapa Commissioners ninawashukuru kwa sababu jana tumekuwa katika Wilaya hii ya Teso kama ilivyo semwa na Co-ordinator wetu kule Malaba na leo tuko hapa na imekuwa shukurani zaidi kwa sababu mumetupa sisi nafasi ya kutoa sauti zetu kufuatana na hii kazi ya Constitution ambayo inaendelea, na mjisikie mko nyumbani na mwendelee kama mpango wetu ilivyo.

Ya pili, sisi kwetu wakaaji wa nyumbani hapa Teso district kama ilivyo semwa na Co-ordinator, kitu kilichoko, tuseme yote. Mtu asiwe na tashwishi kwa mfano: Bwana DO yuko

hapa mnaweza kusema pengine tukizungumza mambo kuhusu serikali DO pengine anaweza kutuchukulia makosa. Si hivyo kwa sababu tunayo tarajia ni mpango ya kesho. Kwa hivyo mtu awe uhuru kuzungumza jinsi anavyotaka, hii Constitution ijayo iwe namna gani? Toa maoni yako kwa sababu ni nafasi yetu kutoa kama hayo.

Kwa hivyo kwa kumaliza, mimi sikujitaja. Mimi ni Councillor Samson Olubayi ambaye ni mwenye kiti wa hapa na si Mwenyekiti wa Teso County Council Bwana Councillor Emodo awa salimie halafu tuone la kufanya.

**Councillor Emodo Moses:** Mwenyekiti wa kikao cha leo, Commisisoners, Bwana DO na Co-ordinator na sisi ambao tumekuja kuwakilisha maneno yetu nasema hamujambo? Mimi ni kukaribisha wageni hawa wenye kuchukua maoni yetu na tuna bahati wamekuja leo hapa kuchukua maoni yetu. Tafadhali tusifiche chochote, tuende kama tumetosheka, yale unaona kama yanakusumbua sana, yale umesema ya Katiba ya zamani ambayo sasa ni mabaya, tengeneza leo wakati huu usije baadaye uende nje na useme ningesema namna hii, hapana. Hawa wamekuja kuchukua maoni yetu, maoni yetu ndio muhimu kwa hivyo nasema karibuni hata mimi nimekuja tutazungumza zaidi kutokana na maneno ambayo nimeandika. Asante sana.

**Charles Engedu:** Sasa ningepatia nafasi hii kwa District Officer wetu aweze kukaribisha Commissioners.

**District Officer:** Thank you very much Dr. Engedu, I would like to take this opportunity to welcome our Commissioners from the Constitution Review team to Chakol division. Just like I told you, this is the one of the divisions that make up Teso district, we have four Administrative divisions. So Chakol is the last one in the Southern part, we border Busia on this other end and we also border Uganda on this other side. I don't want to take much of our time because we are going to dig in for the whole day, I would only like to say this is landmark occasion for our country, it is a very big occasion and because we are trying to re-invent our country for future prosperity. The last time we had the Constitution writing, nafikiri wale wamesoma historia wanajua, tulichagua watu wachache waende kuturepresent kuli Lancaster in England ndio walituchorea Constitution ambayo tuko nayo saa hii. But this one is our own, we are going to invent our future and it is a home grown Constitution that will take the interest and aspirations of all the stakeholders in this country; old men, women, youth, children and the disabled.

I would like kila mtu afanye hili kile tunaita a free discourse, vile mliambiwa na Councillor Olubayi hakuna victimization. The other time nikiwapatia example, wakati watu wa Electoral Commission walikuja to get our opinion on boundaries, on the civic boundaries, we did not give them a hearing si ndivyo? Na walienda, tuliwafukuza. So these boundaries were drawn up in Nairobi and then they came and imposed them on us.

So, let us make use of this opportunity, siku ya leo so that, zile opinions tutatoa leo hapa will be part and parcel of the new Constitution. So I would like to encourage you to be free, utumie ile lugha ambayo unafikiri unaweza kutoa matamshi yako hata kama ni kiteso I think we have interpreters here. Kama ni kiswahili utumie and if you are fluent in English language utumie. So with those few remarks I would just like to welcome the Commissioners to address the gathering. I think I will hand over to Pastor Ayonga who is also the leader of the delegation, may be people would like to know your names first.

**Com. Pastor Ayonga:** Hamjambo! Mimi ninaitwa Pastor Zablon Ayonga, ni mmoja wa Commissioners na ningelipenda kuwa-introduce Commissioners wenzangu ambao tuko pamoja nao. Katika mkono wangu wa kushoto huku mwisho ni Dr. Abdirizak Nunow ambaye siku ya leo atakuwa mwenyekiti...on, nimekosea kidogo atawasalimu atatoa salamu ambazo zime toka huko North Eastern na yeye amebeba salamu za kutoka mbali sana kuzileta mpaka hapa Teso. Wakati ukifika nitampa microphone awasalimie. Hapa kati kati yeye ni jiran tena ni M-western Province huyu ni Bwana John Mutakha Kangu ambaye ata kuja kuwa salimia sijue na lugha ngapi na salamu zake zimetoka hapa karibu lakini ni nyingi.

Na pamoja nasi tuna officer watatu kutoka ofisini ambao wamekuja hapa kufanya kazi maalum. Maalum in a sense kwamba wata-keep records, watanasa maneno ambayo munayo sema na kwamba hakuna neno la mtu ambalo likakalo potea. Ili mjue jinsi ambavyo watakavyo wahudumia, kule kuna Bwana Wanjohi, simama na huyu kwa wale ambao wameleta memorandum zao hebu beba folder yako hicho ni kitu ameleta hapa hata limeandikwa jina lenu hapa . Hakuna neno lenu litakalo potea, maandishi yenu yote yataingizwa kule na pia anayo register. Unapotoa maandishi yako uta-register, utaweka sahihi kuhakikisha kwamba kila jambo limewekwa kule. Na hata wale mtakao zungumza, ambao hamna maandishi itakuwa lazima nawe ujiandikishe kule ujulikane kwamba ulitoa maoni wakati huo. Na ndipo kuna Dada

wawili hapa, hawa wawili mmoja wapo anaandika ni Helen na mwingine ni Grace, yeye Grace anafanya kazi ya kushika maneno. Hakuna neno litakalo potea, hapo mnaweza kuona pengine Dr.Nunow haandiki, Bwana Kangu haandiki na mimi pengine siandiki na unaweza kufikiri “ sasa mimi nililipa kuwa nikiongea, mbona sikuona kama wanaandika? Kumbema maneno yangu yalikuwa ya bure? Hakuna ya hiyo, mambo yote kule ndiko yanakwenda. Hebu inua hiyo mashini waone. Hiyo mashini iko hapo ni ndogo sana lakini ina maana kubwa sana, inashika kila kitu hata jinsi ninavyo sema sasa inanishika kule na sitaweza kuepukana kwamba si mimi nilisema hivyo nilipokua kule Alupe.

Kwa hivyo muwe na uhakika kwamba mambo yenu yote yatashikwa. Kwa hivyo hawa watu wanamaana sana katika kikao hiki. Bila ya kupoteza wakati nataka sasa niwaulize Commissioners wawasalimie, na baada ya kuwa salimia, Commissioner Kangu tutamuuliza atuambie taratibu ili mjuwe ni mpangilio gani uliopo kwa kutoa maoni, utayatawaje na kama kuna dakika ambazo mtu anapewa, utazitumiaje. Na kama umeleta maoni hutaki kuongea juu yake utayafanya aje? Lakini kwanza tusikie salamu zile zimetoka North Eastern.

**Com.Nunuow:** Asante sana com. Ayonga, wananchi wa Teso hasa wa Chakol division Asalaamu Aleykum!

**(Audience)** Waaleykum salaam!

**Com. Nunow:** Yogaa! Asanteni sana. Tunafuraha sana kuwa nanyi, jana kule jijini Malaba tulipata maoni mengi sana na maandishi mengi na ninatumaini leo pia itakuwa hivyo hivyo. Kwa hivyo ukipata nafasi yako zungumza yote unayo moyoni na uzungumze ikiwa hauogopi mtu yeyote, aliyefaa kuogopwa ni Mungu. Na isitoshe, kwa sababu nchi yetu pengine tulizoea uangamizi kadha na kadha na bado watu wanajiona wako kwenye jijini. Lakini hayo mafikira mtoe kwa kichwa, tunaunda Kenya mpya na inatakikana kila mtu aweze kutoa maoni yake bila uoga na upendeleo. Kwa hiyo ninawakaribisha tena na ninge waomba mtoe maoni yenu jinsi mlivyo jitayarisha na utaratibi ambao mtaelezwa na Commissioner mwenzangu. Asanteni.

**Com: Kangu:** Wananchi wa Amagoro Chakol, yoga! Yoga! Sawasawa sasa mimi ninaanza kuelewa ninajua hata majibu mnasema (noi noi) ama hiyo ni ya asubuhi mapema? Wakati wowote, sawasawa. Sasa mimi vile mumeelzwa naitwa Bwana Mutakha Kangu, natoka sehemu za Butere, kwa hivyo mimi ni mtu wa Western Province na leo sio siku yangu ya

kwanza kuingia Amagoro. nimewahi kuwa upande huu kwa maneno ya civic education huko Malaba mara mbili. Tukawasiliana na wale walikuwa huko na leo tunatarajia muko tayari baada ya kujitayarisha kutoa maoni yenu vile mungependelea Katiba ya nchi yetu iwe. Na kama hatujanza vile mumeelezwa kama utaratibu tunafuata na huwa tunapendelea tuwaeleze mapema ndio kila mtu ajuwe akianza asianze kuteleza na kuenda kando.

Jambo la kwanza kuhusu utaratibu ni kwamba, huu mradi ni mradi wa Wakenya wote. Tulisema baada ya kufurugana kwa mda mrefu kwamba tunataka Katiba yenye imetayarishwa na Wakenya wenyewe kupitia njia ya kutoa maoni na kwa hivyo siku ya leo ni siku ya watu wa Amagoro Constituency ikiwa Teso district kutoa maoni. Mko na siku tatu, jana tulikuwa Malaba na leo tuko hapa na Jumatatu tutakuwa Amukura. Isipokuwa jana Mheshimiwa mbunge wenu alitusihi akiomba tungekuwa na kikao kingine karibu na wenzenu wanaoelekea upande wa Mount Elgon tukasema ajaribu kuzungumza na Secretariat, kama atafaulu basi huenda tukawa na kikao kingine huko.

Mkutano wa leo kwa watu wa Alupe, utaratibu wetu unasema mkutano unatakikana uanze saa mbili kamili na kuenda mpaka saa kumi na mbili so mtakuwa na muda wa kutosha isipokuwa naona imeshafika saa nne lakini tutajaribu tuendele. Na maoni tunachukuwa kutoka kwa watu wote, tunataka kujumisha kila mtu; wamama, wazee, vijana, wasichana, watoto, walemavu na watu aina yote.

Tunataka kila mtu apate nafasi ya kujieleza vile angependa mambo yaendeleo, na ikiwa ni mkutano wa Tume ya Kurekebisha Katiba, inafaa mjue mko uhuru. Mkimwona Bwana DO amekaa hapa msifikirie huu mkutano ni wa Bwana DO na kwa hivyo mwogope kusema yale mungependa kusema. Huu ni mkutano wa Tume ya kurekebisha Katiba na mkutano wetu tunasema kuna uhuru wa kila mtu kuzungumza yale yanayomsumbuwa rohoni. Tumesema iko shida yenye inahusu vile tutaendesha maneno ya nchi yetu ndio tukakubalilana kama Wakenya tutafute tujuwe makosa yako wapi na suluhisho litakuwa nini, ndio tukasema watu wapatiwe nafasi ya kuzungumza na ikiwa tumepeana hiyo nafasi na tena nawe uwe na uwoga ukose kutueleza wewe kuelewa kwako unaona shida iko wapi na suluhisho ni nini, hatutakuwa tunafanya yale kulisema tutafanya. Kwa hivyo msogope Bwana DO na hata kama ma- Chiefs wako, wasiogope Bwana DO, yuko hapa hata naye ako na ruhusa ya kutupatia maoni yake,

asifikirie pengine DC atasikia namna gani naye Chief asitulie DO atasikia namna gani, kila mtu akona na uhuru.

Na sisi katika hii kazi tumekuwa tukishirikiana na watu wa serikali na wamejua, wametuhakikishia wametusaikia hawaja kuja ku-interfer na vile maneno yanaenda. So wewe zungumza vile maneno yanaenda mara kwa mara. Nimeambia watu hata kama maoni yako ni kwamba kuna shida na Provincial Administration, elezea hiyo. Usifikirie sababu Bwana DO yuko hapa nikigusa hiyo nitakuwa na makosa, hakuna makosa eleza vile ungependa. Kwa hivyo kila mtu ajisikie uhuru, na ikiwa tunasema kila mtu ajisikie uhuru na tunataka maoni kutoka kwa kila mtu, pia nasi tumasema tunataka tolerance, watu waweze kuvumiliana.

Ikiwa mtu anasimama anazungumza yale wewe hukubaliani nayo, hakuna haja uanze kupiga kelele ama uanze kusema hukubaliani na yeye. Tulia, nyamaza, wacha amalize yake na wewe ukipata nafasi yako utaweza kueleza vile hukubaliani na yule mwenye alikuwa anazungumza kwa jambo, kwa fulani na wewe utuambie kuhusu hilo jambo maoni yako yangukuwa namna gani. Hivyo ndivyo tutaweza kuendelea bila shida mingi.

Na sababu ninasema hivyo ni kwamba mumelezwa tunaandika maneno mnasema na tena tuna nasa mambo hayo na mtambo wa kunasa sauti. Na hatutaki wakati mtu anazungumza mashini inasasa kelele badala ya maneno anazungumza, so patia mtu nafasi ajieleze ndio wewe utapata nafasi yako ya kujieleza.

Na kuongezea hapo tunasema hata kama mtu amesema kile kimekufurahisha sana, ikiwa tunanaza kupiga makofi mara kwa mara tena hiyo ita-interfere na recording yenye tunafanya, ufurahi tu lakini nyamaza aendele ndio the recording process iendele sawa sawa.

Na jambo lingine ni kwamba maoni tunachukuwa kwa namna tatu: namna ya kwanza ni kwamba kuna wale wako na maandishi wameandika mambo yao chini katika memorandum, written memorandum na hawana haja ya kuzungumzia hiyo memorandum ama kueleza hiyo memorandum mbele yetu wanataka kupeana tu. Hawo tunasema ikiwa unashuguli unataka kuenda mahali, hakuna haja ukae unangoja, unaweza toka pole pole uende pale utaandikisha memorandum yako hapo na utoke pole uende. Na ikiwa unataka kukaa kusikiza wengine tena unakaa na kusikiza wengine.

Namna ya pili ni kwamba kuna wale wana maandishi lakini pia wanataka kuzungumzia hayo maandishi, wanataka kuyaeleza, wanataka kufafanua mahali, Tutawapatia nafasi ya



kuzungumza. Lakini tunasema sababu maandishi huenda yakawa mrefu sana, hakuna haja uanze kusoma mambo yote mbele yetu, sababu ni kwamba tuatasoma hayo maandishi yako. Sasa tunataka ukikuja mbele kazi yako itakuwa kumulika yale mambo ya muhimu katika maandishi yako, highlight the most important points bila kutaka kusoma mambo yote. Na ukimaliza tena utapeana hiyo memorandum na utaandikisha jina pale na uweke sahihi.

Namna ya tatu ni wale watu hawana maandishi lakini wako na mambo wanataka kuzungumza ki-mdomo, oral submissions. Hawo tutawapatia pia nafasi ya kuja mbele na kuzungumza na tunaandika na tena tunanasa na hiyo mashini ya kunasa sauti na ukimaliza hata na wewe utatakikana uende uweke sahihi halafu ndio tujue ulipeana maoni yako. Kwa wale wana maandishi, na wanataka kuzungumzia maandishi mara mingi huwa tunasema tunawapatia mda wa dakika tano kwa kujaribu kumulika mambo ya muhimu kwa hayo maandishi.

Na kwa wale hawana maandishi tunawapatia mda wa dakika kumi sababu ikiwa kwamba hawa hawana kitu kingine watatuachia, ni yale wanazungumza na lazima tuweze kupata yote kutoka kwao. Lakini hata hivo tuna- discretion ya kuona kwa sababu kama saa hii naona watu hawajakuwa wengi, tunaweza kuongeza mda. Lakini watu wakianza kuwa wengi na masaa yanaanza kuyoyoma tunaweza aanza kupunguza huo mda.

Pili, tunaweza angalia tuone hata kama uko na maandishi unaweza kueleza na wewe ndio opinion leader mambo yako yamebeba mengi, tunaweza kukupatia nafasi uzungumze mengi ndio tuweze kuelewa kwa sababu unazungumza yale ya watu wengine na wewe pamoja. So hiyo discretion iko, tutaitumia halafu tuone iko namna gani na tukitumia sitaki watu waanze kuwa na wasiwasi ni namna gani, ni kwa nini wanafanya hivi? Na ukimaliza kuzungumza sisi ma-Commissioners tunaweza kuwa na swali moja, mbili kuhusu yale umezungumza, pengine kujaribu kufafanua. Tutakuuliza na ukiwa na jibu utupatie na kama ni jambo hauja fikiria tena sio lazima kujibu, unaweza kutuambia sijawahi kufikiria hilo na pengine nitaenda kufikiria na nione namna gani. So hilo ni jambo lingine inatakikana mjue.

Now, lugha vile mumelezwa tulisema kwa vile huu ni mradi tunataka tuhishe Wakenya waseme mambo yao, hatuwezi kusema tunawapatia nafasi halafu tena tunawanyanganya nafasi kwa kusema tumia lugha fulani kama ni lugha hawawezi kuelewa. Kwa hivyo hatusemi lazima utumie lugha fulani, uko uhuru wewe mwenyewe kuchagua ni lugha aina gani itakuwezesha

kuzungumza mambo yako, kujieleza bila shida. Ikiwa ni Kingereza, ikiwa ni Kiswahili ikiwa ni Kiteso, wewe mwenyewe chagua ni lugha gani unataka kuzungumza na ikiwa ni lugha ambayo mtu atatafsiri tutapata watu wenye watatueleza ni nini mnasema. Kwa hivyo mjisikie uhuru na muweze kuzungumza mambo yenu.

Mkiingia kuna orodha pale mlangoni majina yanaingizwa pale kwa hivyo kuzungumza tutaenda kuita watu tukifuata huo utaratibu ndio tuweze kujua iko namna gani. Kuna kiwango tutafika tukianza kuruka kuita watu wengine tukiwapatia priority kama wazee ama walemavu ama watoto wa shule tunataka waende, msianze kuuliza kwa nini walisema watafuata ordha na sasa tena wanaruka watu wengine. Hiyo discretion tuko nayo na tutaweza kuitumia. Kwa hivyo nafikiria wale wote wako ndani wameandikisha majina pale so that tuweze kuendelea na mkutano.

Na mwisho nataka nitambue kwamba Mayor wa Busia Municipality, Her Worship Lorna Lutta ameingia na ako na na sisi na tuna mkaribisha kwa kukuja kuandamana na sisi. Mimi nimesikia ni mtu wenu huku, so lazima mfurahi, si hiyo ni kweli? Asante. Basi salamia watu kidogo, Mayor.

**Mayor. Lorna Lutta:** Commissioners, DO, Chairman wa County Council na wote wenye wamekuja kwa mkutano wa leo, Hamjambo! Mimi nitasema tu karibuni sana hapa kwetu Alupe na sisi wengine wetu vile tulikuwa na nyinyi kwa Municipal ya Busia, tuko Councillors wa nne tunatoka sehemu ya Amagoro district ambayo inaungana na Municipality. Kwa hivyo nawakaribisha sana na naomba ya kwamba bado asubuhi ni na pia kulikuwa na baridi mingi na tarajia watu watajaa hii hall na wawape nyinyi mawaidha yao kwa uhuru unaowezekana. Kwa hivyo tukianza tusikuwe na shaka ya kwamba watu ni wachache lakini tunawatarajia, wataingia pole pole. Asanteni.

**Com: Kangu:** Asante. Basi tutataka kuanza na tukiita jina lako utakuja hapa mbele na kuzungumza uanze na kutaja jina lako sababu tunataka hata jina lako linaswe kwa mtambo ndio baadaye tukianza kusikiza mambo tujue ni fulani alikuwa anazungumza na vile nimesema ukimaliza hapa unaenda pale kuweka sahihi kwa register. So tuanze na mtu anaitwa Wenseslaus Adungo.

**Wenseslaus Adungo:** Mr. Chairman of this sitting, the Commissioners, my name is Wenseslaus Adungo I was one of the educationist. I have got a short written memorandum, which after reading I will just highlight, the points and then I will submit there.

Sir Chairman I would like to submit a few proposals about the President.

Kenya should have a President aged about 35 years; he should be partyless and should not have a Constituency to represent. The President should serve for 2 terms of 5 years each and retire on pension so that he doesn't come back kung'ang'ania.

Some of the work of the President; he should be Head of State and not Government, He should appoint the Prime Minister and other Cabinet Ministers, who should all be ratified by Parliament. There should a Prime Minister who heads Government.

Constitution supremacy: the Constitution should not be abused by people in power like assonance of decrees unless at the time of emergency. It should be above party politics.

Judiciary: the Judges should be independent and not interfered with by some people. The Government should give legal aid to all people especially those; who cannot pay, in all criminal cases. That one I will clarify; You know in criminal cases some people cannot pay if they are taken to court so the Government should give Advocates/lawyers who do that, but those civil cases, they should be able to pay for themselves.

Defence and National Security: Our borders should be protected properly day and night.

The officers including police should be paid well to avoid bribery so as to protect the country and the Wananchi properly.

Land inheritance: It has been quite difficult to inherit land from the deceased parents. The case goes to court, a lot of expenses are incurred and some people cannot pay all these expenses and will not be able to get the land. This should be verified by the local elders and Chiefs to ascertain the land is his property.

Ethnic minorities: There should be a clause in the Constitution which guarantees that the minority also get a share of the national cake especially when the time of sharing such like

when it comes to voting. You know if it is put if dispute in votes, the minority may not get that one especially in job opportunities, national schools opportunities, representation in the Government and Parastatal bodies. That is all I would like to submit, thank you Sir.

**Com: Kangu:** Thank you Bwana Adungo. Tupate Moses Emodo.

**Moses Emodo:** Mwenye kiti wa kikao cha leo, wana-Commissioners wote, Bwana DO na wananchi ambao wamekuja kuhudhuria, hata sijasahau Mayor ambaye amekuja na sema nataka nianze ili saa isinipite sana.

Mimi naitwa Moses Emodo. Kwanza Katiba yetu ya zamani ni mzuri sana kwani imetuongoza tangu uhuru.

Utangulizi: Ni muhimu kuwa na utangulizi katika Katiba yetu, sisi raia ya Kenya tunataka serikali ambayo inaheshimiwa kumcha Mungu na kuleta mwelekeo mwema wa uongozi, kuelekeza raia kuwa watu wa kutegemea kazi.

Kupangia elimu ya msingi na ya juu bila ubaguzi na mali na kazi kwa wote.

Kulinda maisha ya raia wake.

Kuzingatia sheriya za umoja wa Mataifa za Africa mataifa, za nchi za ma- dollar.

Mwisho, nataka itambuliwe kwamba wenzetu walio pigania uhuru wetu wakumbukwe.

Executive powers: Kenya ni vizuri tuwe na serikali ya mseto ambayo Rais anagawanya mamlaka na Waziri mkuu. Na serikali hii iwe kama ifuatavyo:

- Waziri mkuu awe na kazi ya kuendesha serikali.
- Tuwe na Rais, Makamu wa Rais, tuwe na Waziri mkuu, tuwe na District Commissioners, tuwe na Chiefs na Ass. Chiefs na nafasi ya “Likuru” village elder ibuniwe na awe akilipwa na serikali.
- Ofisi ya Provincial Commissioners isiwekwe na ofisi zozote chini yake, kazi yake inagongana na kazi ya DC. Nafasi ya DC pia isiweko, kazi hiyo inafanywa na machifu vizuri sana.
- Rais achaguliwe na watu, awe Mbunge wa pahali pake. Rais wa nchi awe na miaka arubaini au zaidi na awe ameo. Awe namasomo ya juu ya ziada. Tena ujuzu wa miaka tano kwa serikali na awe na utu, uzalendo. Rais aongoze kwa vipindi viwili viwili vya

miaka tano tano. Rais agawanye mamlaka na Waziri mkuu.

- Local Government: Serikali ya wilaya, hii ni serikali muhimu ambayo ni ya msingi na ya mashinani. Serikali ya Wilaya ipewe uwezo kamili wa kuendesha mabaraza ya wilaya. Mabaraza ya miji zipewe uwezo wa kuajiri na kufuta wafanyi kazi wake. Mayor na mwenye kiti wa mabaraza wachaguliwe na wananchi wote. Vipindi vya miaka tano ndio inafaa kwa Mayor na mwenye kiti kwa kutumikia. Uchaguzi wa Mayor na wenye viti ambao nimetaja juu ugharamiwe na chama saa ya campaign ya kuchaguwa Mayor ama mwenye kiti.
- Wananchi wapewe ruhusa ya kufuta au kurudisha Diwani wao nyumbani akiwa na makosa.
- Mabaraza yasiendele kuwa chini ya Wizara ya serikali za wilaya.
- Diwani awe amesoma mpaka darasa la nane.
- Tume ichaguliwe kuangalia mshahara na marupurupu ya Madiwani na Wajumbe.
- Kuteuliwa kuwoko lakini kwa vikundi maalum kama walemavu, vijana na wanawake.
- Uraia: Kuandikisha kupata kipande kurahisishwe. Mtoto anapozaliwa apate cheti cha kuzaliwa. Mtoto akitimiza miaka kumi na nane cheti hicho kitumiwe na wazazi wa mtoto huyo kupata kipande kuliko kwenda vetting kwenda kwa Chief, hiyo inaharibu na inagharamu pesa mingi. Mtu yeyote ambaye alizaliwa Kenya kabla ya mwaka wa Elfu moja sitini na tatu awe raia kamili. Bibi ya mtu ambaye ni raia wa Kenya na ameolewa na mwanakenya aandikishwe na baada ya miaka kumi apate kipande na awe akipiga kura. Wanakenya wanatakiwa wawe na kipande na passports. Kupata passport pia kuwe rahisi, wakitumia cheti cha kuzaliwa mtu akitaka kusafiri nchi za ng'ambo.
- Polisi wa usalama: Vikosi vyote vya usalama yaani majeshi, AP, GSU, askari wa jela vinundwe kawa Katiba lakini kikosi cha polisi kigawane mamlaka na ma-Chiefs. Kikosi cha polisi kimechukuwa mamlaka mbae sio yake, sheria isiruhusu polisi kufanya masako katika nyumba yako, anatoa uchafu wako wote nje halafu anakubandikia wewe kesi. Polisi wafanye kazi na ma-Chief kuleta uhusiano mwema kati ya polisi na raia. Polisi wa AP wasiruhusiwe kukamata watu kwa sababu hawajasomea sheria ya kushtaki na kukamata mtu.
- Political parties: Vyama vya siasa ni vya muhimu sana kwa kuunganisha raia, vyama zaidi visiandikishwe, viwe tatu peke.
- Njia ipatikane kuongeza uwakilishi wa Wanawake katika Bunge na mabaraza.

- Yeyote akishinda kupata uteuzi kwa chama kimoja aruhusiwe kuhama kwa chama kingine. Lakini mtu akihama akiingia cha kingine kwanza ajiuzulu na aende kupata idhini kwa wananchi.
- Viti vitengwe kwa walemavu, vijana na wanawake.
- Tuwe na uwakilishi wa uwingi wa watu kuliko ukubwa wa sehemu. Kwa mfano; hapa Teso tuna idadi ya watu wengi sana lakini sisi tuna Mjumbe mmoja badala tuwe na Wajumbe wa tatu wa nne kwa sababu tuko wengi na ukifuata njia ya jiogafia ukubwa wa nchi, hatuwezi kuwakilishwa vizuri. Ndio nina decide hapo tuwe na uwingi wa watu, hapo tutapata watu wanao tuongoza vizuri.
- Sehemu za wakilishi ziongezwe kutoka kwa idadi ya mia mbili na kumi hadi mia tatu.
- Uchaguzi wa Rais na Wabunge na Madiwani ziwe siku tofauti, kwa sababu katika nchi zingine uchaguzi wa Madiwani ndio unaanza kwanza ndio chama ambaye ina tawala au ambacho kinaenda kufaulu kinapata nguvu yake kwamba sisi namna gani? Tutafanya campaign namna gani? Kwa uchaguzi wa Madiwani chama kikishinda, chama hicho kitajua pia President wake atakuwa ameshinda.
- Kura zote zihesabiwe pale pale zinapigwa na ushindi utangazwe. Hii imetuletea hasira sana kwa sababu baada ya uchaguzi tunaenda kwa headquarters na tuna kaa karibu wiki moja kura zinaweza kuhesabiwa wiki moja, kabla hamja pata matokeo na halafu pengine kura zingine zinaletwa kwa ujanja, zingine zinatupwa kwa msitu, zingine zinapita kwa njia ingine. Kwa hivyo hiyo itamaliza rigging sana. Siku ya uchaguzi itambuliwe katika Katiba.
- Utamaduni na mila ya Wateso: Wateso wana utamaduni na mila nzuri sana, tumeishi nazo tangu zamani, zingine zimepuuzwa na serikali. Kumbuka asiyependa mila na utamaduni ya kabila yake ni mtumwa. Hatuwezi kuiga mila, tabia, chakula, vinywaji, pombe na nini bila sisi wenyewe kukubali. Katika mila zetu za ki-Africa hakuna sheria inafanywa bila kukula, kukunywa na kucheza. Wizara iangalie ubora wa chakula ikiwa ina wezekana. Mila zetu za utamaduni ambaye nataka zikaguliwe kabisa ni Ektaye( community working together) Epunyas( funeral rites and burials) Akinumunun ( eating new food) Ayare( planting) Ekomrake( marriage and ceremony) Anakimakror( giving a new born child a name) Akisuku( celebrating the new birth). Mwisho Mwenyekiti uniruhusu sasa nisemo ya mwisho.
- Ya mwisho ni forced harambees. Kwetu sisi, neno hili harambee ni neno nzuri sana lakini

watu wamepuuza maana ya neno harambe, harambee imekuwa sasa ni ya nguvu. Tunajua machifuwameambiwa asisanye pesa lakini bado harambee inachukuliwa na kama DC na DO, wanakuja ku-force watu kutoa. Hata ma-Chief wenyewe they are being forced to pay for harambees which are not for them.

- Na kazi, kama ni kiwanda, kama ni factory, ziletwe katika district ili watu waandikwe kazi katika area yao na hii itapunguza ukosefu wa kazi. Na sema asante, ni hayo tu.

**Com: Ayonga:** Bwana Emodo umesema juu ya freedom fighters, wakumbukwe. Unajua kukumbuka utakumbuka, hata sasa tunakumbuka kuna freedom fighters ama there were freedom fighters, lakini hiyo inasaidia nini? Tungelipenda utuambie unataka wakumbukwe namna gani? Kukumbukwa kwa vitendo ndio nafikiri pengine ulikuwa unafikiria?

**Mr. Emodo:** Kwa vitendo.

**Com: Ayonga:** Na vitendo kama vipi?

**Mr. Emodo:** Vitendo kama watambuliwe, wasaidiwe kwa njia nyingine kwa sababu walipigania uhuru, wengine hawana mashamba, wapewe mashamba, wengine wapewe pesa fulani za kujisaidia. Lakini katika maandishi haya ya Katiba, watambuliwe ili watoto wale watakuja, wajukuu wajue uhuru hatukupata bure, walipigania.

**Com: Ayonga:** Asante.

**Mr. Emodo:** Asante pia.

**Com: Kangu:** Asante basi Bwana Emodo. Tupate Donald A. Orkit.

**Donald Orkit:** Kwa majina ni Donald Orkit. Commissioners wetu, DO na wananchi wote wa Chakol division ambao leo wamekuja hapa kwa huu mpango wa utaratibu wetu wa Commission, yangu ambaye naenda kuwakilisha hapa ni juu ya muundo na utaratibu wa uchaguzi. Mfumo ambao unafaa ni ule wa kuchagua Rais kwanza na baadaye uchaguzi wa Bunge na baraza la serikali za wilaya, Councillors wafuate nyuma.

Pia kura ambazo zimepigwa katika kila kituo zihesabiwe hapo papo ili kuzuia kuiba kwa kura, rigging na kisha itangazwe hadharani. Tuendeleo na mfumo kuwa mwenye kura mingi ndiye mshindi, utaratibu huo jinsi ambavyo ulivyokuwa kwa sababu haukuwa ukizuia wanawake kijiunga na siasa. Wale ambao walitaka wame wahi kufanya, kwa hivyo ni wazi kama wanataka, sio lazima kama hawako tayari. Kwa mfano Bi. Ogot na Julia Ojrambo wamewahi

kuonyesha ari yao na wakachaguliwa na wananchi.

Kulingana na asilimia za kura Rais lazima apate asilimia ishirini na tano kutoka kwa miko wa sita ya nchi. Hii itaonyesha amependwa na wengi kuliko hapo awali ambako miko wa tano tu ndizo zilizotambuliwa.

**Com: Ayago:** Endelea kijana.

**Donald Orkit:** Tusiendeele na mfumo wa maeneo ya jiografia ya wakilishi; hatutosheki na ugawaji huo kwa sababu wilaya zingine zinawakishi mmoja Bungeni ilihali zingine zina watu kumi kwa wilaya moja na hata idadi ya watu katika eneo zao ni haba tu.

Bwana Commissioners wetu, hayo ndio nilikuwa nayo. Asanteni.

**Com: Kangu:** Haya tupate Gilbert M. Maase.

**Gilbert M. Maase:** Good morning to you all! I appreciate your presence here the Commissioners. Mine I classified them as oral presentation, I am Gilbert Maase Nengo.

I will start on education. Since we all consider Agriculture as the backbone of our economy, I will say it today that education is the backbone of the economy and on education review some of the things I will prefer to be implemented or to be reflected in our future law are as follows:

- I wish education in primary school to be free. When it comes to colleges and universities, they always charge non refundable fees which I consider should be reported in our law that, it is an illegal activity because we shall have the students from poor families being systematically eliminated from the education process.
- On the parallel degree issue: currently we have seen a situation whereby parallel degree programme is being offered to rich families or people who have other connections. I wish to have the parallel degree programme issue being accommodative of the poor students thus I refer to them being be offered some loans by the Government and that should be part of our law should see to it that the students from all walks of life have access to education. If that is not going to be the case, I recommend that it should be abolished.
- Provincial Administration: I wish to have the DO s and the Chiefs being given full responsibilities or major responsibilities, to be answerable to education status in of any given area. Because we have a very reluctant administration on the part of education and



there is no country that we are going to build if we relax on education. We should put it a priority, the Chiefs to be monitoring who are going to school, which kids are staying at home answers should be obtained from their parents and even the DO should be more concerned with education than any other activity in which we understand they are very much involved.

- Parliamentary issues: Members of Parliament being faced with a vote of no confidence including our Councillors if the voters or the electorate feel that we have picked somebody who is not the right man or woman he or she should be faced with the vote of no confidence and that should be after being forwarded to the Electoral Commission and should be implemented immediately.
- Another issue is on police arrest, we have heard in the past some cases where people are being arrested and there is no information being communicated to the families back home. These people are being held, nobody knows where they are. So we need our law in future to have the police being responsible of the communication issue.
- We need to have as people of Kenya viewing Kenya, as their personal asset. By this I mean we need to have standard moral conducts on all the people. We should have a law that will make sure that we observe our moral standards and we respect Kenya and we have it at our individual level as our personal assets.
- On the banks issue, I will prefer if the banks are not going to make huge profits at the expense of the citizens of this country because currently we have all the banks, according to their reports, doing a very lucrative business which in relation to the people of this country, it does not really reflect that the people of Kenya have economic resources that warrant such successful financial institution prosperity. So we need the borrowing rate to have a minimum range of 2 to a maximum range of 5%.
- The Ministers should be people who have excelled in professional and business fields. We need people like accountants, economist, lawyers, engineers and technicians to be given responsibilities to run the Government ministries and the Cabinet Ministers should not be Members of Parliament. The President should be a professional just like any other Minister who has excelled in politics, management, economics and accounting professions. He should not have absolute powers when appointing Commissions of inquiries. Any who vices for the presidential seats should have a minimum age of 30years.
- Local Administration: We should have a local administration that has clear cut focus on its

activities, they should now venture into revenue or projects that can enable them to generate their own income instead of relying so much on the people or tax payers since we know that poverty line is around 56-56, these people are poor and we need the County Council, the local Government, the Town Councils and the Municipalities to think or to look for professionals who can find out the way forward in future.

**Com: Kangu:** Last point.

**Gilbert M. Maase:** Thank you very much, that is all I had for now.

**Com: Kangu:** Thank you Mr. Maase. Can we have Edson Ng'ang'a?

**Edson Nganga:** Thank you very much. I am Edson Ng'ang'a I'm a teacher by profession and I'm representing Chakol high school community, teachers and students views. I will just give a summary of what I have all the items are on a diskette and I hope you will be able to look at it. But in summary, the community have a feeling that:

- The Government should provide free primary education up to standard 8.
- They feel the current system of education is too tasking and therefore the opinion is that we should revert to the old system of education where we have primary up to standard 7, then secondary education up to form six (6) before you proceed to university.
- The teachers have a feeling that 85% intake during form one selection should be abolished because it is a bit discriminative. All Kenyan students have a right to learn in any secondary school in any part of the country and not to be restricted to their districts.
- Parliament: we feel that any Government that is corrupt, the Members of Parliament should have the powers to impeach it out in case there is misuse of office. We also feel that Members of Parliament should not just be passing bills in Parliament before they consult the views of the Constituents they should come down to the grass root level before they pass any bill.
- On Tax: Kenyans are highly taxed and therefore we feel that the Government should come up with a mode of tax where we are only taxed once, just like our neighbors in Uganda. They use a system known as "Omusolo" I don't know, it is poll tax, something like that. Whereby the Government should be able to asses, individuals, their wealth and taxed them accordingly not being taxed everywhere. In fact the VAT should be abolished.
- We also feel that the President should not have powers to appoint individuals to hold certain

posts but their appointments should be approved by the Parliament or the MPs should vet their appointments. Not only the President, this includes Ministers, Judges and others. Also, any member or any person who has been appointed to a senior Government post or in a Government department he should declare his wealth before he goes into that office because it encourages corruption.

- Road blocks: In this country there are so many, the Government should come up with a mode of trying to minimize these road blocks. They encourage corruption among the police force.
- Lastly, this is a view from students that the issue of rape cases and sexual harassment are very high, those people who are found or who do them should be seriously dealt with.

**Com: Anyonga:** What is the seriousness?

**Edson Nganga:** The law should come up very clearly and define the punishment.

**Com: Anyonga:** But you have to recommend the punishment.

**Edson Nganga:** I think they should be given life sentences because they spoil the lives of those students or those children. And lastly, MPs should not be allowed to decide on their salaries. That there should be a Committee, which should harmonize the salaries of Kenyans. I think those are the few items, there are about 35 items in this diskette. Thank you very much.

**Com: Nunow:** Did you indicate on the diskette the programme that was used to type it?

**Edson Nganga:** Ms word.

**Com: Nunow:** Is it indicated?

**Edson Nganga:** No.

**Com: Nunow:** Please write on it Ms word, it easier the work there as somebody straight goes to the programme straight away.

**Com: Kangu:** Thank you. Can we have Sylvester Ongarapasa Ebu.

**Sylvester Ongarapasa:** Asante sana Commissioners, yangu mimi nimemaliza kuandika zingine lakini nataka kuongeza machache. Jina langu naitwa Sylvester Ongarapasa Ebu.

Yale nataka kuongeza upande wa uchaguzi ya Kenya ili inaendelea saa hii endelea vizuri lakini nataka ibadilishwe Rais awe na siku yake, MP wachaguliwe siku yao. Councilor na siku yake peke yake na wengine pia. Sababu yake, kuna watu ambao wanajipanga kando ya President eti ni wazuri kumbe wao ni kukuja kufuruga wananchi na ndio sababu nataka kila mtu achaguliwe siku yake peke yake.

Halafu ingine, wafungwa pia ni wananchi wa Kenya, nataka pia wapige kura. Tena wagonjwa wale wako hospitali kuna wale wanaweza kutembea na wanaweza kufuhamu pia wapige kura. Sababu kura nyingi zina potea kwa sababu ya kunyima hawa kupiga kura.

Ya tatu kwa upande ya utamaduni wetu tumenyimwa. Naomba serikali ijayo ituwachie utamaduni wetu. Sababu yake sisi Wateso tuko na utamaduni wetu wazee Wateso zamani walikuwa wakikusanyika pamoja na watoto wakielezana 'huyo ndio baba yako, huyo ndio fulani yako'. Sasa wakati huu wamekosa kukusanyika pamoja kwa sababu ya viongozi kukatasa sisi tukae pamoja wakipatikana wazee wakiishi pamoja kuongea maneno ya kimila yao, wanakamatwa na polisi. Na hiyo naomba serikali kidogo ibadilishe ituwachie utamaduni wetu. Nafikiri yangu ni hayo machache yanatosha.

**Com: Kangu:** Asante Bwana Ebu, tupate Pancras Otwani.

**Pancrus Otwani:** Thank you Chairman, my name is Pancrus Otwani and I was a member of Parliament in this area, an Assistant Minister and before that I was a headmaster in one of the biggest schools in the district and then I ended up being a Principal lecturer in teachers college. Well, having been in touch with people, my other views have been expressed and I will not repeat them so I will just touch on few areas that I haven't heard wananchi touch directly.

I will start with the area of Commissions, institutions and offices. My view is that we should adequate Commissions institutions and offices for example, CKRC should stay to guide

whenever amendments are necessary in future because it is inevitable, as we develop, there will be amendments of the Constitution. The Electoral Commission is there, we should have Employment and Ethical Commissions like the Teachers Service Commission that we have, the Public Service Commission and the Parliamentary Service Commission. We should also have the Local Government Service Commission.

Another necessary Commission, in my view, is the lands and boundaries Commission Kenya still has very many touchy issues concerning land and boundaries, so we need such a Commission.

Another Commission, for the promotion and protection of the rights of cultural linguistic and religious communities. And the last one is Human Rights Commission. It is important that these Commissions are free and independent of Executive control and their decisions and recommendations should be fault prove and supreme. Some of them should have the function of setting up codes and regulations for the relevant professions that they serve. Now on that, I would like to suggest strongly that whenever a Commission releases a report, such a report should be implemented immediately because so far we have so many rotting in the archives and wananchi still want to hear what decisions came up on devil worshiping, the tribal clashes the other day, people want to know what happened. The Koech educational report has not yet been released in full. So it is important that those reports are released immediately so that if there is some provision in future to ensure that then the Commissions will have meaning.

- There is one office that I personally think Kenya should establish this time round that is the office of the Ombudsman; call it the public protector like the South Africans do. There Mr. Chairman you will agree with me that the abuse of office in the civil service, parastatals and others is obvious. So far we are dependent on the Parliamentary Public Account Commission to detect some of these issues and suggest necessary action. But they come to the Parliamentary Account Commission too late and I'm very hopeful the officers who are at fault, some of them maybe found dead already, others will manoeuvre their ways. But we need corrections while they are in the office and not when the mistakes have been made and we cannot rectify them any more.
